**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA UCHUMI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA AFISI YA RAIS, FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**Mheshimiwa Spika,**

Namshukuru Mola Mtukufu, aliyetujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana leo hii ndani ya Baraza lako Tukufu kuendelea na majukumu yetu ya Kitaifa. Namuomba Mwenyezi Mungu anijaaliye nguvu katika uwasilishaji wa Hotuba hii na atupe usikivu na uelewa ili tuichangiye kwa umakini bajeti hii iliyopo mbele yetu kwa maslahi ya wananchi. Aidha, napenda kukushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Spika kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu ili niwasilishe maoni ya Kamati ya Uchumi kuhusiana na Fungu F01 Afisi ya Rais, Fedha na Mipango, F02 Mfuko Mkuu wa Serikali na Fungu F03 Tume ya Mipango kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika,**

Nichukuwe fursa hii kumshukuru na kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuiongoza nchi hii kwa weledi, umahiri na adilifu wa hali ya juu. Tunamuomba Mola Mtukufu amzidishiye afya na nguvu ili tuendelee kupata neema tupu ambazo ametuahidi kipindi cha kampeni za kuwania kiti cha Urais katika uchaguzi mkuu uliopita.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa namna ya pekee, naomba kutoa pongezi za dhati kwa Makamo wa kwanza wa Rais Mheshimiwa Othman Masoud Othman kwa kuteuliwa kwake kushika wadhifa huo. Tunamuomba Mola Mtukufu amwezeshe kutekeleza majukumu yake ya Kitaifa kwa ufanisi kwa kufuata nyayo za mtangulizi wake Maalim Seif Sharif Hamad na kuendeleza umoja na mshikamano wa wananchi wetu.

Aidha, Kamati yangu inapenda kumpongeza Makamo wa pili wa Rais Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla kwa jinsi anavyomsaidia Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa majukumu yake ya kuendesha Taifa hili. Ni imani yetu kuwa, kupitia misingi imara ya uimarishaji wa uchumi wetu tutaweza kupiga hatua ya haraka ya kimaendeleo na kuongeza ustawi wa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,**

Nitumie nafasi hii kutoa shukurani za pekee kwa Viongozi na Watendaji wote wa Afisi ya Rais Fedha na Mipango kuanzia Waziri Mheshimiwa Jamal Kassim Ali, Katibu Mkuu Dkt. Juma Malik Akil, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Khamis Suleiman Mwalimu; Kamati inawashukuru sana kwa mashirikiano yao yaliyoiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Wajumbe wa Kamati ya Uchumi walifanya kazi kwa ufanisi mkubwa wakati wa kuipitia bajeti ya Afisi ya Rais Fedha na Mipango mnamo tarehe

27/04/2021 katika Afisi ya Baraza la Wawakilishi. Kwa heshima naomba niwataje Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hiyo kama ifuatavyo:

1. Mhe. Shaaban Ali Othman - Aliyekua Mwenyekiti
2. Mhe. Sabiha Filifil Thani - Aliyekua M/Mwenyekiti
3. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu - Mjumbe
4. Mhe. Shadya Mohammed Suleiman- Mjumbe
5. Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf - Mjumbe
6. Mhe. Juma Makungu Juma - Mjumbe
7. Mhe. Hamza Hassan Juma - Mjumbe
8. Mhe. Hassan Hamad Omar - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,**

Ukamilifu wa kazi hii umechangiwa zaidi na juhudi za Makatibu wetu. Naomba nao niwatambue kwa kuwataja majina yao kama ifuatavyo;

1. Ndugu Asma Ali Kassim Katibu
2. Ndugu Adam Maulid Simai Katibu

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, fungu F01 Afisi ya Rais Fedha na Mipango linakadiriwa kukusanya jumla ya Tsh. 1,783,942,239,000 trilioni kupitia vyanzo mbalimbali vya mapato. Aidha, Ofisi inakadiriwa kutumia jumla ya Tsh. 170,008,366,000 bilioni katika utekelezaji wa programu tatu, programu ndogo kumi na moja na huduma ishirini ilizojipangia.

PROGRAMU YA USIMAMIZI WA BAJETI NA FEDHA ZA UMMA

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati iliarifiwa kuwa mapato yanayotarajiwa kukusanywa kupitia Idara ya Uhamiaji kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kupitia Ada ya usajili wa raia, Ada ya uchunguzi, Ukombozi wa fedha za umma na ada nyenginezo ni jumla ya Tsh. 1000. Fedha hizi haziakisi uhalisia wa mapato hayo na kupelekea Kamati kujiuliza ni kwa vipi Wizara itakusanya Tsh. 1000 kwa mwaka mzima wa fedha? Kwa mnasaba huo, Kamati inashauri makisio ya fedha halisi yaoneshwe kwenye bajeti ya Wizara na kuwepesisha mjadala na kupitishwa kwa vifungu hivyo. Kadhalika, Kamati yangu inapendekeza mapato hayo yanayotokana na Idara ya Uhamiaji kuundiwa kifungu maalumu cha bajeti ili kuweza kuonekana kwa urahisi.

**Mheshimiwa Spika,**

Programu ndogo ya usimamizi wa hazina kupitia huduma ya usimamizi wa Mageuzi ya fedha za umma imekadiriwa kutumia jumla ya Tsh. 116,975,000 milioni. Kamati imeshangazwa sana na uchache wa fedha hizo zikilinganishwa na zile zilizotengwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ambazo ni jumla ya Tsh. 2,200,796,000 bilioni. Ni jambo la kustaajabisha sana kuona kwamba fedha hizo hazilingani na sera ya Serikali ya awamu ya nane kuanzisha mfumo mpya wa usimamizi wa fedha nchini. Hivyo, Kamati inashauri huduma ya usimamizi wa Mageuzi ya fedha za umma kutengewa fedha za kutosha ili kukidhi mahitaji ya usimamizi ya mfumo wa fedha za umma unaotumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa nia ya kudhibiti mapato yetu na matumizi bora kwa maslahi ya umma.

**Mheshimiwa Spika,**

Suala la udhibiti wa fedha na hesabu za Serikali ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa lolote duniani. Kamati yangu inatoa pongezi kwa Afisi ya Rais Fedha na Mipango kwa kuona umuhimu wa kutenga jumla ya Tsh. 1,402,216,000 bilioni kwa ajili hiyo. Wakati wa kupitia bajeti kwenye ngazi ya Kamati, ilibainika kuwa hesabu hiyo iko sawa sawa kwa miaka mitatu mfululizo kuanzia 2021-2022 hadi 2023-2024. Hivyo, Kamati inaitaka Afisi ya Rais Fedha na Mipango kuwa makini sana katika uandaaji wa bajeti yake. Sambamba na hayo, Kamati ya Uchumi inaiagiza Afisi ya Rais Fedha na Mipango kuhakikisha changamoto za kiukaguzi zilizojitokeza mwaka huu zinatafutiwa ufumbuzi ili zisitokee tena kwa miaka ijayo na kupelekea taasisi zote kutumia fedha kwa uadilifu mkubwa.

PROGRAMU YA USIMAMIZI NA UWEKEZAJI WA MALI ZA UMMA

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu imearifiwa kuwa huduma ya usajili wa mali za Serikali haikutengewa fedha kwa ajili ya mwaka ujao wa fedha kutokana na kwamba bado inaendelea na maandalizi ya mfumo wa IT. Hivyo, Kamati inasisitiza juu ya umuhimu wa kukamilishwa haraka miundombinu yote inayostahiki ili hatimae mali zote za Serikali zisajiliwe kwa ajili ya kuzilinda dhidi ya upotevu na matumizi yasiyofaa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, huduma ya Usimamizi wa ununuzi na uondoaji wa mali za Serikali (HF01020201) inakadiriwa kutumia jumla ya

shilingi Tsh. 50,355,000 milioni. Kamati yangu imeshangazwa na kitendo cha kutotengewa fedha kwa huduma hii kwa mwaka uliopita na kutengwa kwa fedha nyingi mno kwa mwaka 2019/2020 bila ya kupata maelezo yanayokidhi haja.

**Mheshimiwa Spika,**

Kupitia programu ya usimamizi na uwekezaji wa mali za umma, Kamati yangu ilifanya ukaguzi kwenye Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar na kujionea utekelezaji wa shughuli zao za kila siku na kushauri mambo yafuatayo:

i. Wizara iekeze kwenye uendelezaji wa nguvu kazi iliyopo kwa kuwaendeleza kielimu watendaji wa mamlaka hii ili kubobea kwenye kazi zao.
ii. Serikali ipitiye upya maslahi ya watendaji wa Mamlaka hii kwa kuifanyia kazi scheme of services yao ili iende sambamba na uzito wa majukumu yao.

**Mheshimiwa Spika,**

Huduma ya usimamizi na tathmini ya mitaji na hisa za Serikali inakadiriwa kutumia jumla ya Tsh. 4,525,525,000 bilioni. Kamati yangu imeshtushwa na upandaji na ushukaji mkubwa (variation) ya fungu la huduma hii kwa miaka mitatu mfululizo (kuanzia mwaka 2020-2021 hadi mwaka 2022-2023 na kujiuliza jee ni kweli mitaji na hisa za Serikali hubadilika mara kwa mara au laa. Hivyo, Kamati inashauri kuwa fedha za huduma hii zipangwe kwa kuzingatia mahitaji halisi ya Serikali katika usimamizi wa mitaji na hisa zake.

PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Jumla ya Tsh. 467,280,000 milioni zinakadiriwa kutumika kwa ajili ya huduma ya utayarishaji na utekelezaji wa bajeti ya Wizara. Kamati yangu inaiagiza Afisi ya Rais, Fedha na Mipango kuzitumia kwa uadilifu fedha hizo na kufikia malengo ya utekelezaji wa bajeti ili kufanikisha mipango ya Wizara kwa maslahi ya Taifa zima.

**Mheshimiwa Spika,**

Kupitia programu ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba, Kamati yangu imepata ukakasi juu ya mradi wa ujenzi wa jengo la Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) Pemba kuhusu mambo yafuatayo:

i. Muda wa mkataba wa ujenzi ambao umekua ukiongezwa mara kwa mara kulingana na maombi ya mkandarasi
ii. Ongezeko la kazi na gharama za ujenzi ambapo jumla ya Tsh. 117,472,017 milioni ziliongezeka baada ya kuongezeka kazi ndogo ndogo kulingana na matakwa ya mjengewa (*client).*

Kupitia bajeti hii, Kamati inaiagiza Wizara kufanya uchunguzi maalum juu ya mradi huu na miradi mengine inayoisimamia ili kutumia rasilimali chache za nchi yetu kwa ufanisi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, fungu F02 Mfuko Mkuu wa Serikali linakadiriwa kutumia jumla ya Tsh. 208,988,800,000 bilioni katika utekelezaji wa programu moja, programu ndogo moja na huduma mbili ilizojipangia.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, fungu F03 Tume ya Mipango linakadiriwa kutumia jumla ya Tsh. 23,154,500,000 bilioni katika utekelezaji wa programu tatu, programu ndogo tisa na huduma kumi na nne. Kati ya fedha hizo, jumla ya Tsh. 12,007,436,000 bilioni ni kwa kazi za kawaida na Tsh. 11,147,064,000 bilioni ni kwa ajili ya kazi za maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa vile Kamati yangu imejadili kwa kina na kuyakubali mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fungu F01 Afisi ya Rais, Fedha na Mipango, Fungu F02 Mfuko Mkuu wa Serikali na Fungu F03 Tume ya Mipango kwa mwaka wa fedha 2021/2022, naomba sasa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu waijadili, watowe ushauri pamoja na mapendekezo yao na hatimae waipitishe bajeti hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa niaba ya Kamati ya Uchumi ya Baraza la Wawakilishi, naomba kuwasilisha.

Ahsante sana,

………………………..,

Sabiha Filfil Thani,

Mwenyekiti,

Kamati ya Kudumu ya Uchumi,

Baraza la Wawakilishi,

**Zanzibar.**